



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2021 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MEI, 2021.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2021.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika. Hali hii iliendelea kuusukuma Ukandamvua (ITCZ) kusogea taratibu kuelekea upande wa Kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilipelekea kupunguza kasi ya upepo uvumao kutoka misitu ya Congo hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya Magharibi mwa nchi.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2021.

Mwenendo wa viashiria vya hali ya hewa hapo juu, vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na pia kusababisha vipindi vifupi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi. Wakati huo huo, vipindi vya mvua nyepesi viliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu Kaskazini Mashariki.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21- 31 MEI, 2021.

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 21- 31 MEI, 2021

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo Kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusogeza ukanda wa mvua (ITCZ) kuelekea

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

upande wa Kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa. Hali hii inatarajiwa kupunguza kasi ya upepo uvumao kutoka magharibi mwa misitu ya Congo hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21- 31 MEI, 2021.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache hususan katika nusu ya kwanza ya dekad.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,): Mvua nyepesi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua nyepesi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya ngurumo za radi, vikiambatana na vipindi vifupi vya mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Kwa Mawasiliano:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S. L. P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz